

# ILANI YA UCHAGUZI YA AZAKI TANZANIA

# AZAKI




Uchaguzi Tanzania
**OKTOBA**
**2015**



## PIGA KURA

UCHAGUZI MKUU TANZANIA
OKTOBA 2015

**Tovuti:** http://www.thrd.or.tz/
**Barua pepe:** thrddefenders@gmail.com
**Sanduku la Posta:** 105926
**Mahali:** Nyumba namba 355, Karibu na Kituo cha Polisi Mabatini,
Kijitonyama, Dar-es-salaam - Tanzania

# YALIYOMO


SHUKRANI ........ iv
MAUDHUI NA MUUNDO WA ILANI ........ v
SIFA ZA KIONGOZI ANAYEFAA ........ vii
SURA YA KWANZA ........ 1
DHANA NA UMUHIMU WA UCHAGUZI ........ 1
1.0 Dhana ya Uchaguzi ........ 2
1.3 Vigezo vya Uchaguzi Huru na wa Haki ........ 5
SURA YA PILI ........ 5
TANZANIA TUITAKAYO ........ 5
2.0 Tanzania Tuitakayo ........ 5
2.1 Mgawanyo wa Madaraka Utawala wa Katiba na Sheria ........ 5
2.1.1 Utawala wa Sheria ........ 6
2. 1.2 Mgawanyo wa Madaraka ........ 8
2.2 Haki za Binadamu ........ 8
Uhuru na Haki za Kiraia ........ 8
2.3 Haki za Makundi Maalumu ........ 11
2.4 Ulinzi wa Rasilimali Muhimu za Nchi na Haki ya Maendeleo ........ 12
2.4 Nafasi na Haki za Asasi za Kiraia ........ 14
2.5 Huduma Za Kijamii ........ 15
2.5.1 Upatikanaji wa Huduma ya Elimu kwa Wote ........ 15
2.5.2 Huduma za Afya ........ 16
2.5.3 Huduma za Maji Safi na Salama ........ 18
2.6 Ushiriki na Ushirikishwaji wa Wanachi katika Maamuzi ........ 18
2.7 Usawa wa Kijinsia ........ 19
2.8 Uchumi Endelevu na Ajira ........ 20
2.9 Uwazi na Uwajibikaji wa viongozi wa Umma ........ 22
2.8 Rushwa, Ufisadi na Ubadhirifu wa mali za Umma ........ 23
SURA YA TATU ........ 25
WITO KWA WADAU ........ 25
3.1 Kwa Wananchi ........ 25
3.2 Kwa vyama vya siasa ........ 25
3.3 Kwa Wagombea ........ 26
3.4 Tume za uchaguzi (NEC/ZEC) ........ 26

3.5 Vyombo vya Ulinzi na Usalama ..... 27
3.6 Wadau wa Kimataifa ..... 27
3.7 Watumishi wa serikali ..... 28
3.8 Vyombo vya Habari ..... 28
3.9 Viongozi wa Dini ..... 28
SURA YA NNE ..... 29
HITIMISHO ..... 29

Uchaguzi Tanzania
OKTOBA
2015

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ANGOZA** | Association of Non-Governmental Organizations in Zanzibar [*Jumuiya ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Zanzibar*] |
| **AZAKI** | Asasi Za Kiraia |
| **CHF** | Community Health Fund [*Mfuko wa afya ya Jamii*] |
| **JUKATA** | Jukwaa la Katiba Tanzania |
| **LHRC** | Legal and Human Rights Center [*Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu*] |
| **FCS** | Foundation for Civil Societies |
| **NEC** | National Electoral Commision [*Tume ya Taifa ya Uchaguzi*] |
| **NHIF** | National Health Insurance Fund [*Mfuko wa Taifa wa bima ya Afya*] |
| **OSIEA** | Open Society Initiative for Eastern Africa |
| **SHIVYAWATA** | Shirikisho La Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania |
| **TAKUKURU** | Taasisi Ya Kuzuia Na Kupambana Na Rushwa |
| **TAMISEMI** | Tawala Za Mikoa Na Serikali Za Mitaa |
| **TCIB** | Tanzania Citizens‟ Information Bureau [*Shirika la Taarifa kwa wananchi Tanzania*] |
| **TGNP** | Tanzania Gender Networking Program [*Mtandao wa Jinsia Tanzania*] |
| **THRDC** | Tanzania Human Rights Defenders Coalition [*Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania*] |
| **WAHAMAZA** | Wanahabari wa Habari za Maendeleo Zanzibar |
| **YPC** | Youth Partnership Countrywide [*Shirika la Ubia wa Vijana Nchini*] |
| **ZEC** | Zanzibar Electoral Commission [*Tume ya Uchaguzi Zanzibar*] |

# SHUKRANI

Wazo la kuweka wazi matakwa ya Asasi za Kiraia (AZAKI) juu ya Tanzania tuitakayo katika mfumo wa ilani ya uchaguzi lilitokana na mkutano wa watetezi wa haki za binadamu uliofanyika tarehe 24/7/2015 kwa lengo la kutathmini nafasi ya Asasi za Kiraia katika michakato ya kidemokrasia ikiwemo uchaguzi mkuu. Mkutano huu uliazimia pamoja na mambo mengine, kuundwa kwa kikosi kazi kitakachoandaa rasimu ya ilani hii kwa niaba ya AZAKI. Inaleta faraja kubwa kwamba, ndoto hii imeweza kutimia na kuwezesha kukamilika kwa ilani hii. Kwa sababu hii, shukrani nyingi ziwaendee wote walioshiriki katika kuibua wazo lenyewe.

Kipekee, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) kwa kukubali kuratibu shughuli nzima ya upatikanaji wa ilani hii katika hatua zake zote. Pia shukrani zetu ziwaendee wajumbe wa timu maalum ya wanaAZAKI kutoka asasi zifuatazo ANGOZA, JUKATA, TCIB, LHRC, SHIVYAWATA, TGNP, THRDC, WAHAMAZA (Zanzibar), POLICY FORUM na YPC, iliyoshiriki katika uandishi wa ilani hii. Aidha, tunawashukuru wote waliojitoa kuweza kupitia na kuhariri kazi hii wakiongozwa na Dr. Helen Kijo-Bisimba. Na kwa umuhimu kabisa, tunatoa shukrani za dhati kwa wakurugenzi wa AZAKI waliokutana tarehe 14/8/2015 kuridhia kwa pamoja kuwa Ilani hii itumike rasmi na AZAKI za Tanzania kuelekea uchaguzi mkuu.

Vile vile, wapo waliowezesha gharama za kuendesha mikutano ya wana AZAKI tangu mwanzo hadi kupatikana kwa ilani hii. Pamoja nao, tunapenda kuwashukuru Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA) ambao walichangia gharama za awali katika kufanikisha kazi hii. Tunatoa shukrani zetu pia kwa Shirika la Foundation for Civil Society kwa kujitolea kubeba gharama zote zilzobaki ili kuhakikisha malengo ya Ilani hii yanafika kwa wadau wote na kwa wakati.

## MAUDHUI NA MUUNDO WA ILANI

Ilani hii ni matakwa ya asasi za kiraia kuelekea na baada ya uchaguzi mkuu kuhusu Tanzania tuitakayo. Ilani hii imetengenezwa kwa ushirikiano wa Asasi za Kiraia(AZAKI) Tanzania na inalenga kutoa mwongozo kwa wananchi na vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kuzingatia Katiba, sheria za nchi na haki za binadamu katika mchakato mzima wa uchaguzi mkuu.

Hivyo basi, ilani hii ni dira na mwongozo kwa wananchi, wagombea, vyama vya siasa, serikali na wadau wengine kuzingatia mchakato wa uchaguzi ulio huru, wa haki na amani. Pia ni mwongozo kwa wanaoomba ridhaa ya kuongoza kuzingatia masuala ya msingi ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yenye tija na maslahi kwa umma kwa maendeleo ya taifa kama yanavyoainishwa katika ilani hii.

**Kimuundo**, ilani hii ina sura kuu nne. Sura ya kwanza inaelezea dhana na umuhimu wa uchaguzi. Sura hii inaelezea kwa ufasaha maana ya uchaguzi na umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa letu. Aidha, sura hii inawafahamisha wananchi uzito halisi wa kura zao na pia kuelezea maana ya uchaguzi huru na wa haki pamoja na vigezo vyake. Vile vile, sehemu hii ya kwanza inaelezea hatua muhimu za uchaguzi na changamoto zake.

Sura ya pili inatoa dira na mwongozo kwa wanasiasa na vyama vya siasa, wanaotafuta ridhaa ya kuwa viongozi kupitia uchaguzi. Hii ndiyo sehemu maalum ya ilani inayoelezea Tanzania tuitakayo. Sura hii inaelezea ndoto za watanzania zinazopaswa kutimizwa na viongozi na serikali itakayoingia madarakani baada ya uchaguzi. Vile vile, inaelezea kwa ufasaha maana ya utawala wa katiba na sheria, mgawanyo wa madaraka, ulinzi na utetezi wa haki za binadamu, ulinzi na matumizi sahihi ya rasilimali za nchi, huduma za msingi kwa jamii, ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za umma na utawala, rushwa na ufisadi, uwajibikaji wa viongozi pamoja na nafasi ya asasi za kiraia katika ulinzi wa haki na kuhimiza maendeleo endelevu nchini.

Sura ya tatu ni mahususi kwa wito wa AZAKI kwa wadau mbalimbali nchini hususani wananchi, vyama vya siasa, wagombea katika uchaguzi, Tume za uchaguzi, vyombo vya ulinzi na usalama, vyombo vya habari, viongozi wa dini, wadau wa kimataifa na watumishi wa serikali kuzingatia ushiriki kamilifu na ulinzi wa amani na haki za binadamu katika mchakato mzima wa uchaguzi na Tanzania tuitakayo kwa maendeleo ya taifa sasa na vizazi vijavyo. Sura ya nne na ambayo ni ya mwisho ya ilani ni hitimisho.

## SISI NI AKINA NANI?

Sisi ni Asasi za Kiraia (AZAKI) za nchini Tanzania zilizoundwa na kutambulika kisheria na zinazofanya kazi katika masuala mbalimbali ya kisheria, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Kwa umoja wetu tunasimamia na kuhimiza utawala wa sheria na haki za binadamu na masuala yote ya kimaendeleo ili kuhakikisha maisha ya mtanzania yanakuwa bora katika nyanja zote. Katika masuala binafsi, kila asasi au kwa makundi yao wanayo ilani inayogusia masuala yao kiasasi, lakini kwa pamoja masuala yote yenye masilahi ya pamoja kama wananchi kwa maendeleo ya taifa tumeyawasilisha kupitia ilani hii ya uchaguzi.

Kwa ujumla sisi ni watanzania, wazalendo, wapenda maendeleo endelevu, watetezi wa haki za binadamu na wasimamizi wa utawala bora na utawala wa sheria.



## SIFA ZA KIONGOZI ANAYEFAA

Uchaguzi ni sehemu kuu ya michakato ya kidemokrasia duniani kote. Sisi asasi za kiraia tukiwa watetezi na wasimamizi wa demokrasia, utawala bora na haki za binadamu, hatumuungi mkono mgombea yeyote wala chama chochote cha kisiasa kinachotafuta kuingia madarakani wala hatulengi kuchukua dola. Kwa ujumla wake, uchaguzi huundwa na wadau wengi lakini makundi makuu mawili ni wapiga kura na wapigiwa kura. Ili wapiga kura waweze kuchagua kiongozi atakayeweza kusimamia maendeleo ya nchi na kuhakikisha amani ya nchi inazidi kudumu haina budi kuwa na vigezo vya kiongozi bora. Vigezo hivyo ndiyo dira inayoongoza asasi zote na wananchi kwa ujumla kuwapigia kura wanaotafuta ridhaa ya kuingia madarakani.

**Kiongozi Anayefaa ni Yupi?**

Hivyo basi, kwa kutambua jambo hilo, Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa umoja wetu tunakumbusha kuwa kiongozi anayefaa kuiongoza Tanzania tuitakayo ni:

- Mtetezi na mlinzi wa katiba na haki za binadamu. Hii ni sifa kuu kwa kiongozi yeyote yule kuanzia ngazi za chini za serikali mpaka ngazi za juu. Kiongozi bora ni yule anayeweza kusimamia, kutetea na kulinda haki za binadamu.
- Awe na utashi na busara za kiuongozi na asiyekubali kupitisha na kusimamia sheria mbovu zenye kukandamiza haki za binadamu.
- Ni muwazi katika utendaji kazi wa serikali na anayethamini ushirikishwaji wa wananchi katika mipango ya umma kwa maendeleo ya taifa. Kiongozi anapaswa kuwa muumini wa maendeleo shirikishi yatakayoweza kuinua uchumi na kuten geneza mazingira rafiki ya ajira.
- Ni muwajibikaji na aliyetayari kufanya maamuzi yenye tija kwa taifa pamoja na kuwawajibisha viongozi wengine wa umma wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao bila kuvunja sheria za nchi.
- Ni mwadilifu, asiyetoa wala kupokea rushwa, mzalendo kwa nchi yake na aliye tayari kuondoa mifumo ya rushwa na ubadhirifu nchini.
- Ni mahiri katika kusimamia na kulinda rasilimali za nchi yetu ikiwemo kupinga mikataba ambayo haina tija kwa nchi yetu.
- Anayeamini kwa dhati katika misingi ya usawa wa kijinsia kwa mapana yake.

## VIPAUMBELE VIKUU VYA AZAKI

(i) **Katiba Mpya**

Tukukumbuke kuwa mchakato wa kuandika katiba mpya ulikwisha anza na umetumia pesa nyingi za Watanzania. Ni wazi kuwa hadi tunapokwenda kupiga kura Octoba 25 mwaka huu mchakato wa Katiba mpya hautakuwa umekamilika, kwa mantiki hiyo sisi wana AZAKI tunawataka wagombea wanaotafuta ridhaa ya uongozi watumie muda wa kampeni kuwahakikishia watanzania kuwa wataendeleza mchakato wa upatikanaji wa katiba ya wananchi ndani ya muda wa miaka miwili. Pia wahakikishie wananchi kuwa watarurudisha misingi ya upatikanaji wa Katiba kwa kuweka mazingira yatakayoheshimu maoni ya wananchi na kujali ushiriki wa wananchi wote katika kutunga Katiba ya Taifa lao.

**(ii) Sera ya Uchumi wa Kitaifa**

Tunataka kiongozi ambaye anatambua kwamba pamoja na kuwa kwenye uhuru zaidi ya miaka 50 watanzania wengi bado ni masikini licha ya kuwa Taifa hili lina utajiri mkubwa. Tunamhitaji kiongozi atakayeweza kuja na sera ya Uchumi wa Taifa yenye malengo ya kulikwamua Taifa kiuchumi kwa kujenga mazigira sawa ya kiuchumi kwa watanzania wote bila kuweka matabaka ya walionacho na wasionacho. Tunahitaji kuona sera ya Taifa ya uchumi itakayosaidia kuliinua Taifa la kutoka kwenye Taifa linalotegemea misaada na kuwa taifa linalojitegemea kiuchumi kwa kuongeza uzalishaji wa ndani, kukuza viwanda vya ndani na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya serikali.

**(iii) Usimamizi wa Rasilimali za Umma**

Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali ambazo ni ardhi, madini, gesi asilia, mafuta, bahari, maziwa, mito, wanyama pori na misitu asilia. Katika miaka ya hivi karibuni ulinzi thabiti wa rasilimali za nchi hususani kwa mamlaka husika umekosekana nchini hali inayosababisha upotevu na ubadhirifu wa rasilimali za nchi kwa mfano, uvunaji haramu wa rasilimali misitu na bahari , umilikishwaji wa ardhi ya wazawa kinyume na sheria pamoja na ujangili wa wanyamapori. Pia tumeona viongozi wakiingia mikataba ya uwekezaji uvunaji na wa rasilimali isiyo na tija kwa taifa. Tunawataka viongozi wote wenye kuwania nafasi za uongozi kutamka bila kificho namna watakavyosimamia na kulinda rasilimali za nchi ili zitumike kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

**(iv) Haki za Binadamu, Utawala wa Sheria na Mgawanyo wa Madaraka**

Tanzania kwa muda mrefu sasa imekuwa na changamoto kubwa kuhusu utawala wenye kufuata misingi ya sheria, haki za binadamu na mgawanyo wa madaraka. Tunahitaji kuona Tanzania yenye viongozi watakaoweza kusimamia utawala wa sheria, kulinda haki za binadamu na misingi ya mgawanyo wa madaraka. Kama njia ya kutekeleza haki za binadamu, pia tunawataka viongozi watakaochaguliwa waweke nguvu zaidi kwenye kuboresha huduma za msingi za kijamii kama vile elimu na afya.

## 1.0 Dhana ya Uchaguzi

Haki za binadamu hususani haki za kisiasa na kiraia zinafafanua uchaguzi wa kidemokrasia kuwa ni mchakato mzima wa kupata viongozi wa ngazi mbalimbali za serikali kwa kuchaguliwa na wananchi. Uchaguzi ni mchakato wa kuwapata viongozi kwa njia ya kidemokrasia kupitia sanduku la kura. Hapa Tanzania kuna aina zifuatazo za uchaguzi kwa mujibu wa Katiba na sheria;

- o Uchaguzi mkuu ambao huwawezesha wananchi kuwachagua vion gozi wakuu wa taifa Rais, wabunge na madiwani kwa Tanzania bara na kwa upande wa Zanzibar huwachagua Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la wawakilishi na Madiwani.
  Uchaguzi wa serikali za mitaa ambao hujumuisha uchaguzi wa wenyeviti wa vijiji, mitaa, vitongoji na wajumbe wa serikali ya kijiji na mtaa. Kwa kifupi, mchakato wa uchaguzi nchini Tanzania unajumui sha;
- o Haki ya kuchagua na kupiga kura ambayo imeainishwa katika ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya Mwaka 1977 (toleo la 2005) na Katiba ya Zanzibar ya 1984 (toleo la 2010).
- o Haki ya kuchaguliwa na kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi kama ilivyoainishwa katika ibara ya 21(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 1.1 Umuhimu wa Uchaguzi

Uchaguzi ni mchakato muhimu sana katika taifa letu kwani ndio hatua pekee ya kidemokrasia inayowezesha kupatikana kwa viongozi wenye jukumu la kuongoza na kuleta maendeleo katika nchi husika kwa kufuata na kutekeleza sera, sheria, kanuni na malengo ya nchi. Kwa ujumla umuhimu wa uchaguzi ni;

- o Kutekeleza dhana ya mamlaka na madaraka yote ya serikali yana tokana na wananchi kama ilivyo ainishwa katika ibara ya 8(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupata viongozi wa nchi kwa ngazi mbalimbali kwa njia ya kidemokrasia.

- Kuheshimu utawala wa katiba na sheria kwa kutekeleza haki zilizoaini shwa katika sheria na Katiba ya nchi.
- Kuwapa nafasi wananchi kushiriki katka shughuli za utawala wa nchi na utekelezaji wa mambo muhimu ya ujenzi na maendeleo ya nchi.
- Kuwapatia wananchi na viongozi fursa ya kujadiliana kuhusu changa moto za maisha ya watu na namna bora ya kuzitatua.
- Ni fursa kwa wagombea kuwasikiliza wananchi na kunadi ilani ya vyama vyao, ikiwa ni pamoja na wananchi kuwawajibisha viongozi wazembe na walioshindwa kutimiza malengo na matarajio ya wananchi.

### 1.2 Umuhimu wa Kupiga Kura

- Kwa kupiga kura, mwananchi anayo nafasi ya kutimiza haki yake ya kikatiba ya kushiriki katika ujenzi wa maendeleo ya nchi na upatika naji wa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi kwa faida yake na vizazi vijavyo.
- Kura inatoa nafasi ya kidemokrasia kwake kama mwananchi kukasi misha madaraka na mamlaka ya kikatiba aliyonayo kwa serikali kupi tia wawakilishi.
- Kura inatoa nafasi kwa wananchi kukasimisha usimamizi wa rasili mali kwa viongozi.
- Kura inatoa fursa kwa wananchi kunufaika na matumizi ya kodi wana zolipa.
- Kura ikitumika vizuri inaweza kutatua matatizo ndani ya jamii.

### 1.3 Vigezo vya Uchaguzi Huru na wa Haki

Uchaguzi unapaswa kuwa huru na wa haki ili kuzingatia demokrasia na utawala wa sheria. Vifuatavyo ni vigezo vya uchaguzi huru na wa haki vina-vyopaswa kuzingatiwa katika mchakato wa uchaguzi nchini;

- Watu wote wenye sifa na vigezo vya kushiriki katika uchaguzi kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi wanashiriki kikamilifu (Universal suffrage).
- Kura inakuwa ni siri ya mpiga kura. (secret ballot)
- Uchaguzi unakuwa wa moja kwa moja yaani kura moja mtu mmoja.
- Usawa unakuwepo na kulindwa baina ya wapiga kura wote na vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi.
- Uwepo wa sheria za uchaguzi zilizo huru na zinazofuata misingi ya demokrasia
- Uwepo wa ushindani wa ukweli wa kisiasa baina ya vyama vya siasa hapa nchini.

### 1.4 Hatua Muhimu za Mchakato wa Uchaguzi

Ili uchaguzi uweze kuwa huru na wa haki lazima mchakato mzima uhusishe hatua muhimu zifuatazo;

(A) Maandalizi ya uchaguzi

- ✔ Utungwaji shirikishi wa sheria za uchaguzi na utekelezaji
- ✔ Uhamasishaji/elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi.
- ✔ Uandikishaji wa wapiga kura unaozingatia vigezo vya kikatiba na sheria za nchi.
- ✔ Kampeni za uchaguzi ili kuwapa wanananchi fursa ya kuchagua kiongozi wanae mtaka.

(B) Wakati wa Kupiga kura

- ✔ Upigaji kura uchaguzi huru, sawa na wa haki
- ✔ Utangazaji wa matokeo ya uchaguzi bila kucheleweshwa.

(C) Baada ya Kura

- ✔ Kukubali ama kukataa matokeo ya uchaguzi
- ✔ Kupinga matokeo ya uchaguzi

### 1.5 Rushwa na Matumizi ya Rasilimali za Umma Kipindi cha Uchaguzi

Matumizi mabaya ya rasilimali za umma kipindi cha uchaguzi ni dhana pana, kwa kifupi ni matendo yaliyo kinyume cha sheria yanayotekelezwa na baadhi ya watumishi wa serikali hasa wale wenye kutaka kuwania nafasi za uongozi, au viongozi wanaotamani kubakia madarakani. Mara nyingi matumizi haya yanatumika kwa lengo la kusaidia viongozi kuendelea kushika dola. Kuna aina mbali mbali ya matumizi ya rasilimali za umma katika uchaguzi kama;

- Matumizi ya rasilimali watu
- Matumizi ya vyombo vya habari vya umma
- Matumizi ya vyombo vya usafiri vya umma
- Matumizi ya fedha za umma
- Matumizi ya mali nyingine za umma

AZAKI zinakemea matumizi mabaya ya rasilimali za umma hasa kipindi cha uchaguzi ikiwa na lengo tu la kusaidia kiongozi au chama fulani kwa kuwa hii ni kinyume na misingi ya kidemokrasia na inaweza kuwa kiashiria kimoja wapo cha uchaguzi usio na usawa na wa haki. Pia tunakemea matumizi ya hongo na rushwa kipindi cha uchaguzi hasa vipindi vya kura za maoni ndani ya vyama na baadaye uchaguzi mkuu.

Matumizi ya rasilimali za umma lazima yafuate misingi ya kisheria, na usawa kati ya vyama vyote vya siasa katika kampeni. Mfano matumizi ya vyombo vya habari vya umma ni vyema vitumike kwa haki.

## 2.0 Tanzania Tuitakayo

Kama sehemu ya kutambua na kuonyesha mchango wetu muhimu kwa maendeleo ya Taifa, sisi wana AZAKI tumeona ni vyema tukatumia fursa hii ya uchaguzi mkuu kuwakumbusha wanasiasa mambo ya msingi ambayo tungependa wayape kipaumbele pindi watakapochaguliwa.

Kwa ujumla, tunapenda kuona Tanzania yenye kuzingatia utawala wa katiba na sheria, kuheshimu haki za binadamu, ulinzi imara wa rasilimali za nchi, watanzania wenye kupata huduma bora za kijamii, taifa lenye kujali uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi katika mambo ya msingi, pia tungependa kuwa na Tanzania isiyokumbatia ufisadi na yenye maendeleo ya kiuchumi ili kutoa ajira na kumaliza umaskini wa watu wake. Sura hii itaeleza kwa kina Tanzania tunayoitaka baaada ya uchaguzi mkuu tarehe 25 /10/2015.

### 2.1 Mgawanyo wa Madaraka Utawala wa Katiba na Sheria

Tanzania kwa muda mrefu sasa imekuwa na changamoto kubwa kuhusu utawala wenye kufuata misingi ya sheria na mgawanyo wa madaraka. Utendaji wa viongozi wengi wa serikali hasa wanapotekeleza majukumu yao ya kiutawala umekuwa wa kutokuzingatia Katiba, sheria za nchi na wenye kukiuka haki za binadamu. Hali hii ya kutokutii na kuheshimu sheria za nchi si tu imekuwa ikijitokeza kwa viongozi bali hata kwa wananchi wenyewe.

#### 2.1.1 Utawala wa Sheria

Utawala wa sheria maana yake ni kuwa raia na viongozi wanaotii na kuheshimu sheria. Sheria zote zinapaswa kutekelezwa na kupitishwa kwa uwazi na ushirikishwaji wa wananchi wote wanaoathiriwa na sheria husika na pia kuhakikisha kunakuwepo na matumizi sahihi ya sheria husika kwa vyombo vyenye jukumu la kutekeleza sheria hizo. Aidha hauna budi kuzingatia nguzo kuu tatu za utawala wa Sheria ambazo ni; Uhalali, Demokrasia na Haki za Binadamu.

**Tamko Kuhusu Utawala wa Sheria**

Ili tuweze kuwa na Tanzania yenye kuheshimu utawala wa sheria, mtu mwenye kuutaka uongozi anapaswa kuwahakikishia watanzania kuwa kutakuwa na Taifa lenye kuuzingatia utawala wa Katiba na Sheria.

- Tunahitaji Taifa ambalo Serikali na watendaji wake pamoja na mtu mmoja mmoja na taasisi binafsi wanawajibika na kufanya maamuzi kwa mujibu wa sheria.
- Kuwepo na sheria nzuri, zinazojulikana na wote, zenye kuzinga tia misingi ya haki, usawa na usalama wa watu na mali zao. Sheria lazima ziwe wazi vya kutosha kwa sababu watu hawawezi kutii sheria ikiwa hawazielewi sheria hizo.
- Tunahitaji Taifa ambalo mchakato wa upatikanaji wa sheria na sera mbalimbali utazingatia uwazi na ushirikishwaji wa jamii na makundi mbalimbali ya raia nchini.
- Tunahitaji mfumo wa utoaji haki ambao ni huru, imara na wenye kuzingatia weledi, muda na usawa mbele ya sheria.
- Tunahitaji Viongozi ambao watawahakikisha watanzania wana pata katiba bora yenye kuzingatia maoni ya wananchi, uwa jibikaji, utawala bora, mgawanyo wa madaraka na haki za binadamu.
- Tunahitaji kuzingatia misingi bora ya Katiba hususani mga wanyo wa madaraka.

**2.1.2 Mgawanyo wa Madaraka**

Serikali ya Tanzania haina mgawanyo sahihi wa madaraka. Tumeona mihimili mikuu ya dola hususani Bunge, Mahakama na Serikali vikiingiliana katika utendaji wake wa kila siku na wakati mwingine mhimili mmoja kukimbia majukumu yake kwa kisingizio cha kuepusha mgongano na mhimili mwingine.Utawala wa sheria unahitaji kuwa mihimili mikuu ya nchi, yaani serikali, bunge na mahakama inatenganishwa na haiingiliani katika utendaji kazi. Kutenganishwa huko kunalenga pia kuzuia watendaji katika chombo kimoja kuwa na majukumu katika chombo kingine.

Kwa mfano, Mbunge kuwa waziri na kushiriki vikao vya serikali katika baraza la mawaziri.

Dhana ya mgawanyo wa madaraka inaeleza kuwa mamlaka ya Serikali ni utendaji; mamlaka ya Bunge ni kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma; na mamlaka ya Mahakama ni kutafsiri sheria na kutoa haki. Hapa Tanzania dhana hii inatajwa kwenye Ibara ya 4(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Tamko kuhusu Mgawanyo wa Madaraka**

- Tunahitaji viongozi watakaohakikisha hakutakuwa na muingiliano wa kimadaraka toka mhimili mmoja hadi mwingine. Mathalani, Serikali kutotawala, kuingilia ama kufanya kazi za mhimili mwingine kama Bunge na Mahakama. Lengo la mgawanyo wa madaraka ni kuongeza ufanisi na kuleta uwajibikaji wa mihimili ya dola.
- Tungependa Tanzania ambayo mawaziri hawatokani na wabunge ili kujenga vizuri dhana ya mgawanyo wa madaraka na uwajibikaji. Ili kuboresha vizuri majukumu ya kila mhimili kusimamia na kuwa jibisha mhimili mwingine ni vyema bunge likawa huru kwa kuto kuwa na mawaziri ili kulipa nguvu ya kuwawajibisha mawaziri pale wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao kulingana na katiba na sheria za nchi.
- Uwepo wa vyombo huru vya utoaji haki hasa mahakama na Tume ya Haki za Binadamu na Tume za Uchaguzi.
- Tanzania yenye mfumo wa uongozi ambao hautoi mwanya kwa watumishi wa umma kushika nafasi za kisiasa.
- Tanzania yenye mfumo wa uongozi ambao hutenganisha shughuli binafsi za kibiashara na uongozi wa umma ili kuepuka mgongano wa kimaslahi.
- Serikali inayoingia madarakani ipunguze mrundikano wa mada raka kwa watendaji wake. Endapo mtu atakuwa Mbunge asiwe mkuu wa mkoa/wilaya wala Mjumbe kwenye Bodi za Mashirika ya umma,

## 2.2 Haki za Binadamu

Mojawapo ya misingi mikubwa ya utawala bora na wa sheria ni kuheshimiwa na kulindwa kwa haki za binadamu. Ili Taifa lionekana kuwa linazingatia misingi ya utawala bora na utawala wa sheria ni muhimu kuheshimu na kulinda haki za binadamu. Haki za Binadamu ni haki za msingi ambazo mwanadamu yeyote yule bila kujali rangi, umri, ulemavu, jinsia, wadhifa, taifa wala kabila anakuwa nazo kama binadamu. Haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Tamko la Haki za Binadamu la mwaka 1948 zimegawanywa katika makundi mbali mbali kama vile haki za kiraia na kisiasa, haki za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni haki za pamoja na haki za makundi mbalimbali.

Hali ya haki za binadamu hapa nchini Tanzania imekuwa siyo ya kuridhisha ingawa kuna maeneo tumeanza kuona mabadiliko madogo madogo. Bado Taifa linakosa uhuru wa kutosha wa maoni na vyombo vya habari kutokana na sababu mbalimbali hususani uwepo wa sheria kandamizi na zinazozuia uhuru stahiki katika tasnia ya habari. Vile vile, wananchi wameendelea kujichukulia sheria mikononi ikiwemo kuua watu wanaosadikiwa kuwa vibaka, kuvamia vituo vya polisi na mauaji ya watu wenye ualbino. Pia kumekuwepo na mazingira magumu ya uhuru wa asasi za kiraia na vyama vya kisiasa kufanya majukumu yao kwa maendeleo ya taifa.

### Tamko Kuhusu Haki za Binadamu

#### (i) Uhuru na Haki za Kiraia

Tunahitaji viongozi watakaozingatia na kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na serikali na vyombo vyake kwa mujibu wa sheria, katiba na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu. Haki hizi ni rahisi sana kutekelezwa na kulindwa endapo tutapata viongozi wenye nia thabiti.

- Serikali inapaswa kukomesha watu kukamatwa kiholela, kuwekwa kuzuizini na kuteswa.

- Haki ya Kuishi imekuwa ikivunjwa sana hapa Tanzania, hivyo tun apenda kuona Tanzania ikipata viongozi wenye kujali na kulinda haki ya kuishi ikiwemo juhudi za kuondoa adhabu ya kifo.
- Tunapenda pia kuona baada ya uchaguzi Tanzania yenye kuzinga tia uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari na kupata habari. Katika kufanikisha hili viongozi watamke kuwa watatoa fursa ya kuzirekebisha ama kuzifuta sheria zote zinazopokonya uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza na haki ya kupata habari.
- Tunahitaji tupate viongozi watakaoweza kudhibiti wimbi la mauaji kwa imani za kishirikina nchini hususani mauaji ya watu wenye ualbino, wanawake na vikongwe.
- Tunategemea kuwa na Taifa lenye kulinda usalama wa watetezi wa haki za binadamu pamoja na waandishi wa habari wanaokuwa katika majukumu yao.
- Usawa mbele ya sheria ni moja ya haki za msingi kwa kila mtanza nia hivyo tunategemea kuwa na Taifa litakalozingatia utoaji wa haki sawa kwa makundi yote.

### **(ii)** Haki za Kisiasa

Haki za Kisiasa ni haki za msingi katika kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika shughuli za umma na utawala wa nchi. Kila raia ana uhuru wa kushiriki ipasavyo katika serikali ya nchi yake moja kwa moja au kupitia wawakilishi wake. Ibara ya 8 na 21 za Katiba zinasisitiza kuwa mamlaka ya nchi yatatoka kwa wananchi na wananchi wana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

**Tamko kuhusu haki za Kisiasa**

- Haki ya Kujumuika pamoja na raia wengine ni mojawapo ya haki za msingi kwa raia wa Taifa lolote lile. Tunawataka viongozi wan aohitaji ridhaa ya kuongoza Taifa hili kuhakikisha haki hii ya kujum uika na kufanya maandamano inalindwa na kuheshimiwa.

- o Kumekuwa na vikwazo katika kusajili na kuendesha vyama vya kiraia na kisiasa hapa nchini. Viongozi wote wenye kutaka ridhaa ya watanzania wanapaswa kuhakikisha kuwa wataweka mazingira rafiki katika kusajili na kuendesha vyama vya kiraia na kisiasa hapa nchini.

- o Wananchi wana haki ya kushiriki katika utawala wa nchi yao. Tunahitaji Taifa litakalotoa mazingira ya uhuru na ushirikishwaji kwa wananchi katika utawala wa nchi. Ili kufanikisha hili, inabidi kuwepo mfumo wa siasa unaotoa fursa sawa kwa wananchi wote na makundi yote ya kisiasa bila ubaguzi au upendeleo. Pia, ili kuwa na uchaguzi huru na wahaki tunategemea viongozi watakaochagu liwa waweke mazingira sawa na wezeshi kwa wananchi kushiriki utawala wa nchi yao. Mathalani kuhakikisha nafasi ya mwananchi kugombea kama mgombea huru inakuwepo.

- o Katiba mpya imekuwa ni kilio cha Watanzania kwa muda mrefu. wa msingi huo tunatoa wito kwa serikali itakayoingia madarakani iwahakikishie wananchi kuwa itapitisha Katiba mpya inayotokana na maoni ya wananchi.

### **(iii)** Haki za Kiuchumi

Haki za kiuchumi mara nyingi hazipewi sana kipaumbele na serikali yetu na zimekuwa zikiwekwa katika sehemu ya malengo muhimu ya serikali kwenye katiba, hali inayoondoa uwezo wa mahakama kuhoji utekelezwaji wake. Haki hizi ni pamoja na haki ya kufanya kazi na kupata ujira stahiki, haki ya kujiunga katika mashirikisho na vyama vya wafanyakazi na waajiri, haki ya kuwa katika hali nzuri kiuchumi, haki ya afya na hifadhi ya jamii na haki ya kumiliki mali. Hali ya haki hizi hapa nchini siyo ya kuridhisha kutokana na kwamba bado kuna changamoto kubwa ya ajira, mazingira magumu ya wafanyakazi, na pia wananchi wamekuwa wakipokonywa haki ya kumiliki mali kama ardhi, mifugo nakadhalika.

**Tamko Kuhusu Haki za Kiuchumi**

- Kulingana na tamko la haki za binadamu la mwaka 1948, haki zote, zinategemeana na zinalingana katika umuhimu wake. Hivyo basi serikali inapaswa kupitisha katiba mpya iliyotokana na maoni ya wananchi inayowapa wananchi uwezo wa kuhoji utekelezwaji wa haki hizi za kiuchumi kama ilivyo kwa haki za kiraia na kisiasa.
- Serikali inapaswa kuhakikisha inaweka sera, mpango mkakati na vipaumbele vinavyotekelezeka kuhusu kunyanyua hali ya uchumi kwa wananchi wasio na ajira hususani kutengeneza mazingira rafiki ya ajira kwa sekta rasmi na wale wanaojishughulisha kwenye ajira zisizo katika mfumo rasmi, ikiwemo kilimo, uvuvi na ufugaji.
- Serikali inapaswa kuhakikisha Sheria za ardhi zinazohitaji wanan chi kushirikishwa pale ardhi inapotwaliwa na serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo na uwekezaji zinatekelezwa.
- Kuwepo na fidia stahiki na ya wakati kulingana na bei ya soko baada ya ardhi kutwaliwa kwa mujibu wa sheria.

**2.3 Haki za Makundi Maalumu**

Haki za makundi maalum ni haki zote zinazojumuisha haki zote za binadamu katika makundi mbalimbali ya watu wanaotakiwa kupewa uangalizi maalum kwa sababu ya hali ya mazingira magumu wanayokutana nayo katika jamii. Makundi haya ni kama vile watoto, vijana, watu wenye ulemavu, wakimbizi, wazee, wanawake na makundi mengine madogo madogo katika jamii.

Kwa kuwa haki za watu walio katika makundi haya zimeainishwa katika haki za binadamu, kumekuwepo na usahaulifu wa mamlaka husika na wananchi kwa ujumla kuwa makundi haya yanahitaji uangalizi maalum kulingana na mazingira wanayokutana nayo katika maisha. Mathalani, mauaji ya watu wenye ualbino nchini, sheria kandamizi dhidi ya wanawake na watoto na pia ukosefu wa hifadhi ya jamii kwa wazee na makundi mengine ya pembezoni.

**Tamko Kuhusu Haki za Kiuchumi**

- o Serikali inayoingia madarakani ihakikishe inapitisha katiba mpya iliyotokana na maoni ya wananchi inayoainisha haki za makundi maalum na wajibu wa serikali na jamii nzima kuhusu makundi hayo maalum.
- o Utekelezaji thabiti wa mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo Tanzania ni nchi mwanachama iliyo mahususi kwa ajili ya watoto, wazee, wakimbizi, watu wenye ulemavu, wanawake, vijana na makundi ya pembezoni kama vile wafugaji asilia na waokota matunda.
- o Serikali kupitisha sera na sheria madhubuti inayowalinda watu wenye ulemavu na isiyo ya kibaguzi pamoja na kuhimiza na kuwe ka miundo mbinu iliyo rafiki kwa watu wenye ulemavu wote kufu rahia haki zao za msingi za kikatiba.
- o Kuondoa au kurekebisha sheria zote na sera kandamizi dhidi ya wanawake na watoto.
- o Kuahakikisha jamii za makundi madogomadogo hasa zilizo pem bezoni mwa nchi na zilizosahaulika zinalindwa na zinapewa fursa ya kunufaika na rasilimali za nchi.
- o Serikali ihakikishe inatekeleza sera za wazee na vijana kwa kutu nga sheria zitakazo simamia na kulinda haki zao.
- o Serikali ihakikishe inaweka mazingira mazuri ya wafugaji asilia na wakulima wadogo wadogo kutumia rasilimali za nchi ili kupun guza migogoro ya mara kwa mara.

## 2.4 Ulinzi wa Rasilimali Muhimu za Nchi na Haki ya Maendeleo

Haki ya ulinzi na hifadhi ya rasilimali muhimu za nchi ni moja kati ya haki muhimu katika makundi ya haki za binadamu hususani haki za kiuchumi na haki za pamoja. Hivyo basi, dhana ya utawala wa sheria na haki za binadamu,ni lazima izingatie ulinzi na matumizi ya rasilimali za nchi kwa maendeleo ya taifa.

Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali ambazo ni ardhi, madini, gesi asilia, mafuta, bahari, maziwa, mito, wanyama pori na misitu asilia.
Katika miaka ya hivi karibuni ulinzi thabiti wa rasilimali za nchi hususani kwa mamlaka husika umekosekana nchini hali inayosababisha upotevu na ubadhirifu wa rasilmali za nchi kwa mfano, uvunaji haramu wa rasilimali misitu na bahari , umilikishwaji wa ardhi ya wazawa kinyume na sheria pamoja na ujangili wa wanyamapori. Pia tumeona viongozi wakiingia mikataba ya uwekezaji, uvunaji wa rasilimali usiyo na tija kwa taifa. Tunawataka viongozi wote wenye kuwania nafasi za uongozi kutamka bila kificho namna watakavyosimamia na kulinda rasilimali za nchi ili zitumike kwa manufaa ya Taifa na watu wake.

**Tamko Kuhusu ulinzi wa rasilimali za nchi**

- Mamlaka husika katika serikali itakayoingia madarakani zizingatie na kutekeleza mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni mshirika inayoelezea haki ya ulinzi wa rasilimali kwa manufaa ya wananchi wote na wananchi kufaidi rasilimali muhimu zanchi,kama ilivyo ainishwa kwenye ibara ya 21 ibara ndogo ya 1 ya mkataba wa Afr ika wa haki za binadamu na watu.
- Kuwapa wananchi mamlaka ya kikatiba ya kushitaki serikali maha kamani pale viongozi wanaposhindwa kusimamia ipasavyo rasili mali za nchi.
- Sheria zote zisizolinda rasilimali muhimu au zinazotoa mwanya kwa rasilimali za nchi kutumika bila kumnufaisha mwananchi zifu twe au kurekebishwa.
- Serikali ijayo isimamie vizuri uvunaji, matumizi na mgawanyo sa wa wa rasilimali za nchi ili kuepuka migogoro baina ya wawekezaji na wananchi pamoja na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kama vile migogoro ya wakulima na wafugaji.
- Kuwepo na uwazi wa mapato, matumizi na mikataba inayohusu uwekezaji kwenye rasilimali za nchi kama madini, gesi, mafuta ardhi, misitu na wanyama pori.

- Mamlaka za nchi zizingatie, kutekeleza na kusisitiza juu ya matumizi mbadala ya nishati kama gesi ili kunusuru uhai wa misitu asilia na kuepusha hali ya jangwa nchini. Kwa mfano, gesi asilia iliyovumbuliwa Mtwara itumike Kwa manufaa ya wananchi wote na sio kunufaisha wawekezaji pekee.

**2.4 Nafasi na Haki za Asasi za Kiraia**

Asasi za Kiraia zimekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa. AZAKI zimekuwa mstari wa mbele kutetea haki na maslahi ya watanzania wote. Mara kwa mara, baadhi ya viongozi wa taifa hili wamekuwa hawathamini mchango na kazi za AZAKI hadi kuzipa majina mbalimbali kwa lengo la kuzichafua. Asasi za Kiraia hazipewi kipaumbele kama wadau muhimu wa maendeleo katika Taifa hili. Uhuru wa AZAKI kufanya kazi zao umekuwa pia ukipata vikwazo vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa sheria kandamizi na vizuizi vya kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo, ulinzi wa haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji.

**Tamko Kuhusu Nafasi ya AZAKI**

- Tunataka viongozi watakaochaguliwa wazingatie umuhimu wa kutambua na kulinda nafasi ya AZAKI kama wabia muhimu wa maendeleo na utawala bora wenye kuzingatia sheria katika Taifa.
- Wawe tayari kufanyia marekebisho au kuondoa kabisa sheria mbalimbali zinazokandamiza uhuru wa AZAKI na watetezi wa haki za binadamu hapa nchini.
- Kukemea baadhi ya viongozi wanaotumia nyadhifa zao kukandamiza na kuzuia utekelezaji wa kazi za AZAKI katika maeneo yao.
- Tunataka viongozi watakaoshirikisha AZAKI katika mipango mbalimbali ya maendeleo na kuthamini michango ya AZAKI kwa ustawi wa jamii na Taifa.
- Viongozi watakaotoa uwakilishi wa AZAKI katika vyombo vya maamuzi kama Bunge bila kupitia chama chochote cha siasa. Mfano Rais kutumia madaraka yake ya uteuzi wa wabunge kumteua mwakilishi wa AZAKI asiyefungamana na chama chochote.

## 2.5 Huduma Za Kijamii

Huduma za jamii ni haki za msingi katika kujenga jamii yenye maendeleo endelevu.Kwa mujibu wa Katiba, serikali inapaswa kuweka mazingira wezeshi kuhakikisha huduma za kijamii zinapatikana kwa urahisi na kwa watu wote na kwa wakati. Huduma hizi ni kama vile elimu, afya, maji safi na salama. Kwa miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru hali ya utoaji wa huduma za msingi za kijamii umekuwa sio wa kuridhisha. Katika kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma hizi nchini, wananchi wote wanapaswa kushirikishwa katika mipango na maamuzi kuanzia ngazi za chini hadi ngazi za juu.

### 2.5.1 Upatikanaji wa Huduma ya Elimu kwa Wote

Haki ya elimu ni haki ya msingi ya binadamu na ni haki muhimu kwa maendeleo. Haki hii inahamasisha uhuru na uwezo wa mtu binafsi katika kujiletea maendeleo. Bado miundombinu ya shule zetu za msingi, sekondari na vyuo hairuhusu upatikanaji wa elimu bora na endelevu kwa mustakabali wa Taifa. Ubora wa elimu hapa nchini kwa ngazi zote umekuwa ukishuka kutokana na sababu mbalimbali zikiwepo ukosefu wa walimu wenye sifa na wakutosha, miundo mbinu mibovu, ukosefu wa vitabu vya ziada na kiada, vifaa vya kufundishia na mazingira magumu ya kazi na uratibu na usimamizi mbovu wa sekta ya elimu.

**Tamko Kuhusu Elimu**

- Tunahitaji viongozi na serikali itakayo kuja na Dira ya Elimu na kuweka mikakati endelevu ya kuboresha kiwango cha elimu kwa manufaa ya watanzania wote.
- Viongozi waweke mazingira bora ya kutolea elimu inayozingatia mahitaji ya makundi maalum na watoto wenye mahitaji maalum. Kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanakwenda kwa kupiga vita ajira kwa watoto wenye umri wa kuwa shule.

- o Tunamtaka kiongozi atakayejali na kuboresha mishahara na mas lahi ya walimu na kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa walimu kwa shule za sekondari na msingi.
- o Kiongozi atakayechaguliwa asimamie na kuondoa tofauti kubwa za ubora kati ya shule za serikali na zile za binafsi.
- o Tunawataka viongozi watakaochanguliwa kufuta sheria za kibaguzi zinazominya fursa ya mtoto wa kike kupata elimu, baadhi ya sheria hizo ni pamoja na zinazochangia mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri mdogo.
- o Tunahitaji kiongozi atakaye hakikisha kuwepo kwa usawa wa kijin sia katika sekta ya elimu.
- o Viongozi watakaoingia madarakani wahakikishe kunakuwepo na miundo mbinu rafiki ya kujifunzia kwa watu wote ikiwemo watu wenye ulemavu.

### 2.5.2 Huduma za Afya

Haki ya kiwango stahiki cha maisha inatambuliwa chini ya Ibara ya 25 (1) ya Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, ikiwepo; “Kila mtu ana haki ya kiwango cha maisha kinachokidhi afya na ustawi wake na familia yake, pamoja na chakula, mavazi, makazi na matibabu na huduma muhimu za jamii……..”

Hali halisi ya upatikanaji wa huduma za afya nchini Tanzania hairidhishi hivyo kuathiri haki ya kuishi. Bajeti ya Taifa kwa kipindi cha miaka zaidi ya 10 haija-kidhi azimio la Abuja la kutenga kiasi cha asilimia 15 ya fedha za ndani kwa ajili ya bajeti ya afya. Pamoja na kuwa na mipango mbalimbali ya utekelezaji, uzoefu umeonyesha kuwa fedha zinazotengwa na serikali hazifiki kwa wakati ili ziweze kutekeleza majukumu mbalimbali ya afya. Hivyo kutokana na hali hiyo sekta ya afya imekuwa na hali mbaya kwa kukosa watumishi wa kuto-sha, vifaa tiba, miundombinu mibovu na mishahara midogo.

**Tamko kuhusu huduma za AFYA**

- o Tunataka serikali itakayoingia madarakani kuondoa tatizo la kulip ishwa fedha za matibabu wanawake wanaojifungua katika zaha nati za kata na hosiptali za umma. Tungetaka kuona serikali itakayo ingia madarakani ikitenga fedha za kutosha kwenye bajeti yake kwa ajili ya sekta ya afya ili kuboresha huduma za afya iweze kufikia au kuzidi aslimia 15 zilizopendekezwa na Azimio la Abuja.
- o Tunataka kuona watu wanaoishi na ulemavu, virusi vya UKIMWI, watoto chini ya umri wa miaka mitano nao wapatiwe huduma za afya nzuri na za kutosha bure kwa hospitali zote.
- o Tunahitaji kuona uongozi utakaohakikisha kuwa magonjwa kama saratani na shinikizo la damu yaingizwe kwenye mfumo wa kupata matibabu kwa njia ya Mfuko wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii (NHIF na CHF ).
- o Tunataka serikali ijayo iboreshe utaratibu wa wazee na watoto kupata matibabu ya bure.
- o Watanzania wanahitaji uongozi utakao okoa maisha ya wananchi masikini kwa kupeleka wataalamu wa kutosha wa afya maeneo yote hasa ya vijijini.
- o Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe inajenga nyumba za wafanyakazi kwenye zahanati zote nchini ili kusogeza huduma karibu na wananchi.
- o Tunahitaji kuona viongozi watakaohakikisha watu wenye ualibino wanapata vifaa vya kujikinga na magonjwa na mionzi kama vile mafuta maalum ya ngozi na miwani ya jua.
- o Tunahitaji kuona utaratibu wa huduma za matibabu nje ya nchi unakuwa wazi na unatolewa bila upendeleo. Pia serikali iboreshe huduma za afya hapa nchini ili kupunguza gharama za matibabu nje ya nchi.
- o Tunahitaji viongozi watakaolinda haki za mlaji wa madawa na vyakula dhidi ya madawa na vyakula vyenye madhara kiafya na kiwango duni.

### 2.5.3 Huduma za Maji Safi na Salama

Huduma ya maji ni moja wapo ya huduma za msingi kwa maisha ya binadamu kwa kuwa maji ni uhai. Sera ya maji ya mwaka 2002 inaeleza kuwa madhumuni ya jumla ya sera kuhusu utoaji wa huduma ya maji ni kuboresha afya ya jamii na kusaidia kuondoa umaskini vijijini ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa maji safi salama na yakutosha.Hata hivyo hali halisi ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa mijini na vijijini imekuwa tatizo sugu.

**Tamko kuhusu huduma za MAJI**

- Tunataka kuona viongozi watakaochaguliwa wakihakikisha kuwa tatizo la wanawake wa mijini na vijijini kutembea umbali mkubwa kutafuta maji linapatiwa ufumbuzi.
- Maji yawe ni kipaumbele cha serikali ijayo na kuhakikisha bajeti ya maji inaongezwa ili kukidhi mahitaji.
- Maji yasiwe bidhaa Kama ilivyo sasa, iwe ni huduma ya msingi na serikali ihakikishe wananchi wote wanaipata bila tatizo.
- Serikali ihakikishe inasimamia vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira kwa kutoa elimu.

### 2.6 Ushiriki na Ushirikishwaji wa Wananchi katika Maamuzi

Kuna changamoto mbalimbali zinazokabili utendaji wa mamlaka ya serikali za mitaa hadi serikali kuu. Hadi sasa mamlaka ya wananchi imeporwa na haijulikani ipo wapi. Haieleweki ni namna gani wanashiriki katika maamuzi na katika shughuli za maendeleo na ukuaji wa uchumi wa nchi, huduma za Jamii na maisha yao kwa ujumla. Tanzania ya leo, inahitaji kiongozi atakayesimamia na kuweka mikakati thabiti ya uanzilishwaji na utekelezwaji wa mpango wa uboreshaji wa mfumo wa serikali za mitaa ulioanza mwaka 1998 ambao ulilenga kupeleka madaraka kwa wananchi. Miradi mbalimbali ya maendeleo imekosa ushiriki kamilifu wa wananchi katika hatua za awali za uibuaji na usimamizi.

**Tamko kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi:**

- Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe inaboresha sheria za serikali za mitaa ili ziweze kuwawajibisha viongozi wa vijiji/mitaa ambao hawashirikishi wananchi kwenye zoezi la kuibua, kupanga na kusimamia miradi katika maeneo yao
- Viongozi watakaoingia madarakani waweke utaratibu utakaozi bana serikali za mitaa/serikali kuu kuheshimu maamuzi ya vikao halali vya serikali za mitaa/vijiji vilivyobainisha vipaumbele vya wananchi na hivyo ndivyo vipewe fedha kwa utekelezaji
- Miongozo ya usimamizi wa rasilimali za umma iliyotolewa na TAMI SEMI isimamiwe na kutekelezwa kikamilifu ili wananchi washiriki kuwawajibisha viongozi wabadhirifu wa rasilimali za umma.
- Kuhakikisha wananchi kuanzia ngazi ya vijiji/mitaa kupitia serikali zao wanashiriki ipasavyo katika kutunga sera za nchi badala ya kuwa watekelezaji tu.
- Serikali itakayoingia madarakani iwaelimishe wanachi kuhusu ulipaji kodi na ihakikishe inakusanya kodi na kutumia mapato ya kodi hizo kwa manufaa ya wananchi.

## 2.7 Usawa wa Kijinsia

Dhana ya usawa wa jinsia inatumika pale ambapo jamii imeweza kuondoa pengo lililojengeka katika kufikia, kumiliki na kufaidi rasilimali zinazoshikika na zisizoshikika katika jamii husika. Kimantiki usawa wa jinsia ni hali ya maisha isiyojengeka katika kubagua mwanamke au mwanaume kutokana na jinsi au hali yake.

Hapa kwetu Tanzania usawa wa jinsia unapanuka kwa kasi ndogo na hivyo kudhoofisha demokrasia na kuathiri maendeleo yetu hususani vita dhidi ya umaskini. Azimio la Umoja wa Afrika kupitia Mkataba wa Nyongeza wa Maputo uliagiza nchi wanachama kufanya marekebisho ya Katiba ili kuwezesha kufikia 50/50 usawa wa kijinsia katika Uongozi ifikapo mwaka 2015.

**Tamko kuhusu usawa wa KIJINSIA**

- Serikali itakayoingia madarakani ihakikishe inawezesha kufikiwa kwa lengo la 50/50 kwenye nafasi zote za uongozi
- Viongozi watakaochaguliwa wadhibiti mfumo unaoruhusu wenye mali kuhodhi madaraka ya kisiasa ambao unadhohofisha demokra sia shirikishi, na kuadhiri ushiriki wa Wanawake na wanaume masikini katika maamuzi ya uongozi wa taifa lao katika ngazi zote.
- Kuweka utaratibu wa kisheria na kikatiba utakaotoa mwongozo kuwezesha makundi yote ya jamii kama wanawake, makundi ya pembezoni na wenye ulemavu wa viungo wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi kama wapiga kura na kama wagombea uongozi wa nyadhifa mbalimbali.
- Kupiga marufuku matumizi ya lugha za kashfa , matusi, udhalil ishaji kwenye chaguzi zote ili makundi yote yaweze kushiriki bila kikwazo.
- Tunataka serikali ambayo itarekebisha au kuondoa kabisa sheria kandamizi kwa haki za mtoto na mwanamke kama ile sheria ya Ndoa ya 1971.

## 2.8 Uchumi Endelevu na Ajira

Haki ya kupata ajira ni haki inayotambulika kikatiba, na serikali inalo jukumu la kuhakikisha kuwa inaweka mazingira safi na rafiki ili kumpa nafasi mwananchi kunufaika na haki hiyo. Hata hivyo, ajira bado ni changamoto kubwa sana Tanzania. Pamoja na ongezeko la wasomi nchini, pia ahadi za viongozi mbalimbali wa serikali kuweka mazingira bora ya ajira baada ya kuingia madarakani, serikali na taasisi za umma zimekuwa hazitoi kipaumbele na kusisitiza upatikanaji kwa wingi wa ajira na kutokuweka mazingira rafiki ya kujiajiri, hali inayosababisha hali mbaya ya kiuchumi kwa watanzania wengi hasa vijana.

Kilimo ambacho kinaajiri watanzania zaidi ya asilimia 80 bado hakijaweza kuwakwamua wananchi walio wengi ambao wameendelea kuishi katika hali isiyoridhisha kiuchumi kwa kuwa wengi wao ni wakulima wadogowadogo na wamekua wakitumia mbinu na nyenzo duni zisizo endana na teknolojia ya kilimo cha kisasa. Pamoja na kuwa serikali tangu kupata uhuru imekua na kauli mbiu na mikakati mbali mbali ya kuendeleza na kukuza sekta ya kilimo kama vile "siasa ni kilimo", "kilimo ni uti wa mgongo" na pia kwa sasa "kilimo kwanza", bado kauli mbiu hizi hazijaweza kubadilisha hali kwa kuwa hazikutekelezwa ipasavyo.

Tofauti na kilimo sekta nyingine za uchumi zinazoweza kusaidia kuinua ajira nchini ni utalii, uvuvi, usafiri, mawasiliano, viwanda na biashara, uchimbaji madini na kadhalika. Kwa kiwango fulani, baadhi ya sekta kama za usafiri zimeweza kuwaajiri vijana wengi ingawa bado wanafanya kazi katika mazingira magumu.

**Tamko kuhusu ajira na Uchumi**

- Tunahitaji kuwa na viongozi wenye mipango na mikakati thabiti na inayotekelezeka ya kufufua na kuendeleza kilimo cha kisasa na endelevu kwa kutumia umwagiliaji na nyezo za kiteknolojia za kilimo cha kisasa.
- Inahitajika mikakati ya wazi ya namna viwanda vitakavoboreshwa nchini kwa kuanza na viwanda vidogo vidogo vya kuongeza tham ani ya mazao ya kilimo kama vile vya kusindika matunda, ufungaji korosho na senene, ufugaji wa nyuki na uhifadhi wa madafu na vinginevyo ili kuhakikisha kuwa kilimo kinakuza ajira na uchumi kwa kusafirisha mazao nje ya nchi.
- Viwanda vilivyokuwa vikizalisha mazao kama vile nguo, nyama, minofu ya samaki, pamba na vinginevyo vifufuliwe na kuanza kufanya kazi tena.

- o Mazingira rafiki ya kujiajiri yatengenezwe ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wananchi kwa kuwapa mitaji, kurahisisha masharti ya kukopa pesa na nyenzo muhimu, pia kuweka mitaala ya ujas iriamali na kilimo bora cha kisasa katika mfumo wa elimu nchini kuanzia ngazi za chini hadi vyuoni.
- o Kuboresha maslahi ya wafanyakazi na wananchi waliojiajiri katika sekta binafsi kwa kuwapa motisha.

**2.9 Uwazi na Uwajibikaji wa viongozi wa Umma**

Ili shughuli za umma ziweze kutekelezwa vema kwa maendeleo ya taifa zima, mazingira ya kisheria na kiutendaji yanapaswa kuwa shirikishi na wazi. Bila jambo hili, uwajibikaji wa viongozi na wananchi hautawezekana. Katika nchi yeyote inaofuata misingi ya kidemokrasia, uwazi na uwajibikaji wa viongozi wa umma na wananchi kwa ujumla ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi.

Viongozi wa serikali kutokuwa wawajibikaji na kukithiri kwa usiri wa maamuzi na shughuli zenye manufaa kwa umma imekuwa ni jambo la kawaida sana nchini. Bunge ambalo ni mhimili mkuu unaotakiwa kuisimamia na kuiwajibisha serikali kwa mujibu wa Katiba umekuwa haupewi nafasi ya kushirikishwa katika maamuzi mengi yanayofikiwa na serikali, hasa mikataba mbalimbali ambayo serikali inaingia kuhusu masuala ya uwekezaji katika rasilimali za nchi. Hali hii imesababisha kukithiri kwa ufisadi, ubadhirifu na kukasimisha rasilimali za nchi kwa wageni, hali isiyowanufaisha wananchi na taifa kwa ujumla.

Aidha, kumekuwepo na mtindo wa kupeleka miswada ya sheria bungeni kwa hati ya dharura kwa masuala muhimu kama uhuru wa habari na haki ya kupata taarifa, na miswaada ya rasilimali ya gesi na mafuta. Hali hii ni usaliti kwa watanzania.

Katika nchi ambayo wananchi hawako katika mazingira mazuri ya kupata taarifa kwa wakati kama Tanzania, inashangaza kuwa serikali inafurahia kuendelea kuficha taarifa za msingi za utekelezaji wa shughuli za umma, sera na sheria muhimu za nchi kwa maendeleo ya taifa la leo na vizazi vijavyo.

**Tamko Kuhushu Uwazi na Uwajibikaji**

- Tunahitaji viongozi ambao watatetea uwazi na uwajibikaji serika lini na katika mihimili ya dola. Hii itakuwa ni pamoja na kuhakiki sha kuwa miswada mbalimbali ilyoandaliwa kama vile ya sheria za haki ya kupata taarifa na uhuru wa habari na sera zake zitape lekwa bungeni kwa muda mahsusi baada ya maoni ya wananchi.
- Tunataka kuona viongozi wanapitisha na kulinda katiba mpya itokanayo na maoni ya wananchi.

**2.8 Rushwa, Ufisadi na Ubadhirifu wa mali za Umma**

Tanzania katika siku za karibuni imeshuhudia kushamiri kwa tatizo la rushwa, ufisadi na matumizi mabaya ya mali za umma uliosababisha kudidimiza sana uchumi wa nchi. Rushwa ni matumizi mabaya ya madaraka au nafasi aliyenayo mtu kwa ajili ya kujinufaisha. Pia, inahusisha kitendo cha kumpa mtu aidha pesa, hali au mali ili akupe upendeleo fulani. Pia Taifa linakumbwa na tatizo la ukusanyaji na usimamizi mbovu wa mapato yatokanayo na kodi.

Wakati wa uchaguzi na hata baada ya chaguzi kumekuwepo na vitendo vya rushwa vilivyokithiri hapa nchini hali inayosababisha ukosekanaji wa haki na kudumaa kwa maendeleo ya Taifa. Kwa ujumla wake, ufisadi unajumuisha maovu au uharibifu wa namna yoyote ile ikiwemo matumizi mabaya ya ofisi za umma au binafsi kwa manufaa ya mtu binafsi au kundi la watu.

Nchini Tanzania, ingawa kuna sheria zinazodhibiti matumizi ya pesa au mali binafsi au ya umma katika chaguzi, sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa na pia taasisi maalum kwa ajili ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU), utekelezaji wake umekuwa si wa kuridhisha sana hali inayo-sababisha kushamiri kwa vitendo vya kifisadi hasa kwa viongozi wa serikali na umma huku wananchi wakiendelea kuwa mafukara.

**Tamko kuhusu Rushwa, Ufisadi na Ubadhirifu wa Mali za Umma**

- Tunatakaa kuona sheria za kuzuia na kupambana na rushwa wak ati wote zinatekelezwa kikamilifu na wahusika wanachukuliwa hatua stahiki.
- Tunahitaji kuona uhuru na uwazi wa taasisi za kuzuia na kupam bana na rushwa katika utekelezaji wake wa kazi. Hii ni pamoja na kuweka wazi ripoti za rushwa na ufisadi nchini.
- Tunataka kuwa na kiongozi mwadilifu, anayechukia rushwa, mwe nye mikakati thabiti ya kuondoa tatizo hili na aliyetayari kuwaji bika pale itakapobainika amehusika kwa namna yoyote ile katika ufisadi.
- Tunataka kuwa na Taifa linaloweza kumaliza rushwa kwenye ukusa nyaji wa kodi na hatimaye kukusanya kodi toka kwa makundi yote hasa makampuni makubwa ya uwekezaji badala ya kuendelea Ku muumiza mtanzania kwa kodi mbalimbali huku wakitoa misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa.

### 3.1 Kwa Wananchi

- Wananchi ndio wadau muhimu katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Octoba 25 mwaka huu, hivyo wanapaswa kushiriki kikamilifu katika mikutano yote ya kampeni kusikiliza sera za wagombea wote wa vyama vya siasa ili wakati wa kupiga kura wafanye maamuzi sahihi.

- Viongozi wabovu huwekwa madarakani na raia wema ambao huwa hawajitokezi kupiga kura. Hivyo tunawahimiza wananchi waliojiandikisha wajitokeze kwa wingi siku ya kupiga kura na kutimiza wajibu wao.

- Aidha wananchi wasikubali kwa hali yoyote kurubuniwa na wanasiasa na kupoteza haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka. Baada ya serikali ya awamu ya tano kuapishwa wananchi wawe tayari kushiriki hatua zote za michakato ya maendeleo badala ya kuwaachia wanasiasa kuamua na kutekeleza wenyewe.

- Ni lazima kufuatilia Kwa karibu ili kuweza kuwawajibisha viongozi na watendaji wote ambao hawatimizi majukumu na ahadi zao wakati wote.

### 3.2 Kwa vyama vya siasa

- Vyama vya siasa vinapaswa kuendesha kampeni za kistaarabu zinazoheshimu misingi ya sheria na siasa za ushindani ambazo zinatambua kuwa kuna kushinda na kushindwa.

- Kusiwepo na kampeni za vitisho, matusi na ubaguzi wa aina yoyote na badala yake kuwepo kampeni za kistaarabu zinazoheshimu na zinazozingatia maadili ambayo vyama vyote vya siasa vimesaini.

- Vyama vihakikishe vinasambaza ilani zao za uchaguzi kwa wingi kwa wananchi. Pia, chama kitakachoshinda kiunde serikali na kuipa jukumu la kutekeleza ahadi zote zilizoandikwa kwenye ilani ya chama chao.

### 3.3 Kwa Wagombea

- Tunawasihi wagombea wajikite kwenye ajenda za wananchi sambamba na ilani za vyama vyao na kuacha kuwahadaa wananchi kwa ahadi ambazo wanajua hawataweza kuzitimiza.

- Tunawataka wagombea waache tabia ya kutumia pesa kuwahonga wananchi na njia nyingine zisizostahili kwa lengo la kujipatia madaraka.

### 3.4 Tume za uchaguzi (NEC/ZEC)

- Tume za uchaguzi zifanye kazi kwa uhuru, kufuata sheria, kusimamia kanuni walizokubaliana na vyama vya siasa na kujiepusha kwa namna yoyote kukipendelea chama chochote wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

- Tume zinapaswa kuhakikisha kuwa zimewapa mafunzo ya uhakika maofisa na wasidizi wa uchaguzi na kuchunguza mienendo yao kabla hawajawakabidhi vituo vya kazi ili kuepusha makosa yaliojitokeza wakati wa kuandikisha wapiga kura.

- Tume za Uchaguzi zinapaswa kufanya maandalizi mapema, pia kusambaza vitendea kazi vinavyotakiwa kwa wakati ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza siku ya upigaji kura.

- Tume zihakikishe kuwa watu wote wenye sifa na kustahili kupiga kura ambao hawakuandikishwa kupiga kura kwa sababu mbali mbali ikiwemo wanafunzi wanaandikishwa katika daftari la kudumu la kupiga kura na wanapiga kura.

### 3.5 Vyombo vya Ulinzi na Usalama

- Vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi zake kwa uweledi na tahadhari ya kutowatia hofu wananchi na wapiga kura. Vyombo vya ulinzi visitumie vitisho, nguvu, na silaha za kivita wakati wa mikutano ya kampeni na siku ya kupiga kura.

- Vyombo vya usalama havipaswi kwa namna yoyote kuegemea upande wowote wa chama cha siasa bali vitende haki kwa vyama vyote na wananchi wote wakiwemo wagombea mmoja mmoja na wala visikubali kuyumbishwa na mamlaka yoyote nje ya sheria inayovipa mamlaka kutekeleza wajibu wao.

- Tunalishauri Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutojihusisha na mchakato wa uchaguzi kuanzia kipindi cha maandalizi, cha kampeni, upigaji kura na baada ya upigaji kura.

### 3.6 Wadau wa Kimataifa

- Wadau wa kimataifa waendelee kuzisaidia serikali zetu kitaalamu na kifedha ili ziweze kufanikisha mchakato wa uchaguzi huru na wa haki.

- Wadau wa kimataifa waendelee kufanya kazi kwa karibu na Asasi za kiraia ili kufanikisha utoaji wa elimu ya uraia na mpiga kura kwa wananchi.

- Wadau wa kimataifa wajiepushe kuingilia masuala ya ndani ya vyama vya siasa.

### 3.7 Watumishi wa serikali

- Watumishi wa serikali wanaogombea nyadhifa mbali mbali za kisiasa wasiruhusu na wasitumie mali za umma wakati wa michakato yote ndani ya vyama vya siasa na hata wakati wa uchaguzi mkuu.

- Watumishi wa umma wawe huru wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu na pia watumie haki yao ya kikatiba kuwachagua viongozi wanaowataka bila ya kupokea shinikizo na vitisho kutoka kwa mtu yeyote ndani na nje ya serikali.

### 3.8 Vyombo vya Habari

- Vyombo vya habari na waandishi wa habari wafuate na kuzingatia maadili ya taaluma yao kwa kuhakikisha taarifa wanazozitoa kwa umma hazipendelei chama au mgombea yoyote bali zilenge kuchambua sera za vyama na tija yake kwa wananchi.

- Aidha, vyombo vya habari vya umma vinavyoendeshwa kwa kodi za wananchi vihakikishe kwamba vinawapatia fursa sawa wagombea na vyama vyote vya siasa.

### 3.9 Viongozi wa Dini

- Viongozi wa dini wanapaswa kuhubiri amani kwa wafuasi wao na kujiepusha na kutamka kauli zenye muelekeo wa kupendelea mgombea au chama fulani kwenye maeneo yao ya ibada, majukwaani na hadharani. Hata hivyo wanaweza kutoa ushauri au elimu ya uraia kwa waumini wao na taifa pasipo kuegemea itikadi yoyote.

# HITIMISHO

Sisi Asasi za Kiraia tukiwa ni sehemu ya wananchi na wapiga kura, tunatoa ilani hii iwe ni dira na mwongozo kwa wananchi, wagombea, tume za uchaguzi, vyombo vya ulinzi na usalama, vyama vya siasa na wadau wengine hapa nchini.

Ni imani yetu kuwa ilani hii itatumika katika kuhakikisha tunakuwa na mchakato wa uchaguzi ambao ni huru, wa haki na usiokuwa na matumizi ya nguvu, rushwa, hongo na matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma.

Aidha, tunayo imani pia kuwa, wagombea, vyombo vya habari, viongozi wa dini na wadau wengine wataepuka lugha za chuki na kibaguzi na uchochezi wa aina yoyote. Kwa kufanya hivyo, Tanzania itaweza kupata viongozi wanaoheshimu utu, haki za binadamu na kuwajibika kwa wananchi ambao ndio msingi kwa wananchi wanaowatumikia kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi.

